**REPUBLIC OF KENYA**

**THE SAMBURUCOUNTY ASSEMBLY**
**THIRD ASSEMBLY**
**(THIRD SESSION)**
**REQUEST FOR STATEMENTS**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu 45(c), naomba kauli kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sekta ya Huduma za Matibabu, Afya na Usafi kuhusiana na msongamano wa wagonjwa katika wodi ya wazazi ya kituo hicho.

**Mheshimiwa Spika,**

Katiba ya Kenya inahakikisha kila mtu ana haki ya kiwango cha juu zaidi cha afya kinachoweza kupatikana, ikijumuisha haki ya huduma za afya, ikiwemo huduma za afya ya uzazi (Kifungu cha 43(1)(a)). Aidha, Jedwali la Nne la Katiba linaeleza kuwa serikali za kaunti zinawajibika kwa huduma za afya za kaunti, ikiwemo huduma za afya ya msingi, huduma za ambulensi, na uendelezaji wa afya ya msingi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kuzingatia masharti haya ya kikatiba, ninasimama mbele yenu kuleta suala la dharura la umma kuhusu hali ya wodi ya wajawazito katika Hospitali ya Rufaa ya Kaunti ya Samburu. Imenifikia taarifa kuwa hospitali hiyo inakabiliwa na msongamano mkubwa, hasa katika wodi ya wajawazito. Wajawazito wanalazimika kushiriki vitanda baada ya kujifungua, hali ambayo si tu inawanyima faraja bali pia inaweka hatarini afya ya mama na mtoto mchanga.

**Mheshimiwa Spika,**

Zaidi ya hayo, kumekuwa na ripoti nyingi za uzembe na uvivu miongoni mwa wafanyakazi wa afya katika hospitali hiyo. Uzembe huu katika utoaji huduma umewaacha wagonjwa wengi wakiwa na hasira na kutoridhika na huduma wanazopokea. Hali kama hizi hazikubaliki na zinahitaji hatua za haraka.

**NAOMBA KAMATI HII ITOE MAJIBU KATIKA MAMBO YAFUATAYO:**

1. Sababu za msongamano katika wodi ya wazazi na kupendekeza suluhisho za haraka za kupunguza tatizo hili.
2. Uzembe na uvivu ulioripotiwa miongoni mwa wafanyakazi wa afya kwa kutekeleza hatua kali za usimamizi na uwajibikaji.

3. Rasilimali za kutosha zinatengwa ili kuboresha miundombinu na uwezo wa wodi ya wazazi kukidhi mahitaji yanayoongezeka.
4. Mafunzo ya mara kwa mara na programu za maendeleo kwa wafanyakazi wa afya ili kuboresha ujuzi wao na kujitolea kwao katika utoaji huduma.

**SAINI: ..........................................**
**MHESHIMIWA SARAH LEKIRENYEI,**
**MWAKILISHI WA KAUNTI ALIYETEULIWA (NOMINATED MCA)**
**TAREHE: ..........................................**